# TARGETER KCPE JARIBIO LA TATU STAHIKI

## DARASA LA NANE - 2020

**STAHIKI 003**

## KISWAHILI:
## SEHEMU YA KWANZA: LUGHA

**Muda: Saa 1 Dakika 40.**

### MAAGIZO KWA WATAHINIWA
### SOMA MAAGIZO YAFUATAYO KWA MAKINI .

1. Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibu. Kijitabu hiki kina maswali 50.
2. Ikiwa utataka kuandika chochote ambacho si jibu, andika katika kijitabu hiki.
3. Ukiisha kuchagua jibu lako, lionyeshe katika **KARATASI YA MAJIBU** na wala **sio** katika kijitabu cha maswali.

**JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU.**

4. Tumia penseli ya kawaida.
5. Hakikisha ya kwamba umeandika yafuatayo katika karatasi ya majibu:

**NAMBARI YAKO YA MTIHANI**
**JINA LAKO**
**JINA LA SHULE YAKO**

6. Kwa kuchora kistari katika visanduku vyenye namba zinazokuhusu, onyesha namba yako kamili ya mtihani (yaani nambari ya shule, na zile namba tatu za mtahiniwa) katika sehemu iliyotengwa mwanzo wa karatasi ya majibu.
7. Usitie alama zozote nje ya visanduku.
8. Iweke safi karatasi yako ya majibu, na usiikunje.
9. Kwa kila swali **1-50**, umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi **A, B, C, D**. Ni jibu **MOJA** tu kati ya hayo manne ambalo ni sahihi. Chagua jibu hilo.
10. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.

**Mfano**

**Katika kijitabu cha maswali: Kamilisha tanakali ya sauti ifuatayo**

**18.** Pepesa macho ____________

A. pepepe.
B. rapurapu.
C. kupekupe
D. twaa

Jibu sahihi ni **C**

Katika karatasi ya majibu

16. [A] [B] [C] [D]  17. [A] [B] [C] [D]  18. [A] [B] [C] [D]  19. [A] [B] [C] [D]

**18,** kisanduku chenye herufi **C** ndicho kilichochorwa kistari.

11. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako kiwe cheusi na kisijitokeze nje ya kisanduku.
12. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku **kimoja** tu kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

**Kijitabu hiki cha maswali kina kurasa 8 zilizopigwa chapa.**

*Huchapishwa na kuratibiwa na taasisi ya uchapishaji ya Targeter Educational Publishers Ltd.*
*Email: info@targeterpublishers.co.ke*

**GEUZA UKURASA**

*Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne hapo. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.*

Samani___1___Bidii zilimfanya___2___. Watu walitoka karibu na mbali kujionea___3___. Biashara yake ilinawiri kwa___4___udugu ambao ni___5___. Hakuwa na___6___maadamu___7___aliyemwomba msaada, alimsabilia kwa mengi. Alijaribu kusaidia kulingana na uwezo___8___. Hata wahenga walisema___9___.

1. **A.** aliyeunda **B.** iliyounda **C.** zilizounda **D.** alizounda
2. **A.** ajulikane kama mwanaharamu **B.** ajulikane kama pesa **C.** atambulikane kama ugonjwa **D.** ajulikane kama kazi
3. **A.** viti, vitanda na makabati **B.** masanduku, milango na bawaba **C.** malango, nyua na mabeseni **D.** paa, kuta na mabati
4. **A.** kudhamini **B.** kuthamini **C.** kutweza **D.** kuvunja
5. **A.** hali ya kuwapenda walio karibu na wenzenu **B.** hali ya kutaka msaada wa wengine **C.** hali ya kupenda kushirikiana na wengine **D.** hali ya kutaka kuhudumiwa na wenzako
6. **A.** mkono mzito **B.** mkono birika **C.** mkono kono **D.** mkono wazi
7. **A.** yoyote **B.** wowote **C.** yeyote **D.** zozote
8. **A.** zake **B.** chake **C.** lake **D.** wake
9. **A.** kutoa ni moyo usambe ni utajiri **B.** cha mwenzako si chako **C.** hiari yashinda utumwa **D.** mtu hujikuna ajipatapo

___10___limevamia maeneo___11___ya nchi. Wakulima wengi___12___hasara isiyo kifani. Lazima serikali ichukue hatua za haraka___13___baa la njaa___14___. Inasemekana wadudu hawa wana uwezo wa kulifanya eneo ___15___kuwa jangwa.

10. **A.** Biwi la nzige **B.** Wingu la nzige **C.** Sisisi ya nzige **D.** Mkururo wa nzige
11. **A.** mengi **B.** nyingi **C.** mingi **D.** vingi
12. **A.** wanakadiriwa **B.** wanakadirisha **C.** wanakadiria **D.** wanataka
13. **A.** kwa hivyo **B.** hivyo basi **C.** hata hivyo **D.** la sivyo
14. **A.** itaonekana **B.** itashuhudiwa **C.** litashuhudiwa **D.** zitaingia
15. **A.** lolote **B.** yoyote **C.** zozote **D.** zote

*<u>Kutoka swali la 16 mpaka 30, chagua jibu lililo sahihi.</u>*

**16.** Ni jibu gani lenye mpangilio sahihi wa aina za maneno katika sentensi ifuatayo?

*Wazazi wetu ni wachochezi kuliko wenu*

A. Nomino, kivumishi, kitenzi, kivumishi, kihusishi, kiwakilishi.

B. Nomino, kitenzi, kiwakilishi, kivumishi, kihusishi, kivumishi.

C. Nomino, kivumishi, kiunganishi, kivumishi, kihusishi, kiwakilishi.

D. Nomino, kielezi, kitenzi, kihusishi, kiunganishi, kivumishi.

**17. Chagua usemi halisi wa sentensi hii**

*Kamau alisema kwamba wangeenda kuogelea siku ambayo ingefuata*

A. "Tutaenda kuogelea kesho," Kamau alisema.

B. "Mtaenda kuogelea siku inayofuata," Kamau alisema.

C. "Nitaenda kuogelea kesho," Kamau alisema.

D. "Utaenda kuogelea siku inayofuata," Kamau alisema.

**18.** Hii ni tamathali gani iliyotumiwa hapa?

Kelele zake zingeitetemesha dunia

A. Nahau.

B. Sitiari.

C. Chuku.

D. Tashbihi.

**19. Chagua wingi wa**

*Baharia huyu hodari ni mgeni huku kwangu*

A. Baharia hawa hodari ni wageni huku kwetu.

B. Mabaharia hawa hodari ni wageni huku kwetu.

C. Mabaharia hawa hodari ni wageni huku kwangu.

D. Baharia hawa hodari ni wageni huku kwangu.

**20.** Badilisha sentensi ifuatayo katika kauli ya kutendewa

*Omari alienda mtoni akayachote maji ya nyanya*

A. Maji ya nyanya yalichotwa mtoni na Omari.

B. Omari alimchotea nyanya maji yake mtoni.

C. Mtoni kulichochotwa maji ya nyanya na Omari.

D. Nyanya alichotewa maji mtoni na Omari.

**21. Unganisha sentensi hizi mbili**

*(i) Tuliivunja safari ya kwenda ughaibuni.*

*(ii) Hali ya usalama haikuwa shwari.*

A. Tuliivunja safari ya kuenda ughaibuni licha ya hali ya usalama kutokuwa shwari.

B. Tuliivunja safari ya kwenda ughaibuni mathali hali ya usalama haikuwa shwari.

C. Tuliivunja safari ya kwenda ughaibuni minghairi ya hali ya usalama kutokuwa shwari.

D. Tuliivunja safari ya kwenda ughaibuni ilhali hali ya usalama haikuwa shwari.

**22.** Chagua sentensi yenye kiwakilishi cha pekee.

A. Mtoto huyu ni wangu, huyo ni wako.

B. Kitabu kingine kitatumika kufanya mazoezi.

C. Embe zuri limeliwa ilhali baya limetupwa.

D. Wengine watasafiri kwa ndege mpya.

**23.** Ni jibu lipi linaloonyesha sifa iliyoundwa kutokana na nomino?

A. Mcheshi - cheka

B. Kimbia - mbio.

C. Kilimo - ukulima.

D. Imani - aminifu.

**24.** Chagua jibu linaloonyesha aina za mashairi

A. Mizani, tathmina.

B. Tarbia, ukwapi.

C. Uteo, ukwapi.

D. Tathlitha, tarbia.

**25.** Chagua neno ambalo lina silabi changamano

A. Umuhimu.

B. Hakika.

C. Mtajo.

D. Mazingira.

**26.** Kiambishi **-ka-** kimetumiwa kuleta maana gani katika sentensi ifuatayo?

*Atapelekwa ng'ambo akaendeleze masomo yake.*

A. Kuonyesha kitendo kimoja kinasababishwa na kingine.

B. Kuonyesha nia ya kufanya jambo fulani.

C. Kuonyesha hali ya kuamrisha.

D. Kuonyesha vitendo vinavyofanyika pamoja.

**27.** Chagua sentensi yenye 'O' rejeshi awali.

A. Raia walimao shamba hili ni wa asili ya Kichina.

B. Maembe yanayopatikana shambani humu ni mazuri.

C. Bawabu alindaye pale ni askari wa magereza.

D. Mchwa wajengao kichuguu ni wale wa kiume.

**28.** Andika kwa maneno $\frac{7}{3}$

A. Subui tatu.

B. Theluthi tatu.

C. Sudusi tatu.

D. Theluthi tatu.

**29.** **Maana ya methali**

*"Bura yangu sibadili na rehani,"* ni

A. Jambo ambalo unaliona rahisi kwako kwa mwenzako huenda likawa gumu.

B. Hufai kudharau kitu chako duni kwa kutamani cha mwenzako.

C. Haifai kuwadharau watu waliokusaidia hapo awali huenda ukawahitaji baadaye.

D. Kitu unachokiona duni kwako huenda kikawa na manufaa kwa mtu mwengine.

**30.** Sehemu ya nyuma ya wayo ni

A. kiwiko.

B. kisugudi.

C. kiganja.

D. kisigino.

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali **31** mpaka **40.***

Nyumbani kwetu, nilikuwa mwanambee. Hivyo basi nilifaa kuwa kielelezo bora kwa wanuna wangu. Kinaya ni kuwa wanuna wangu ndio waliotumiwa kama mfano bora. Jambo hili likawa kichocheo cha mimi kugura nyumbani. Hapo nikawa kati ya wale watoto sugu wa kutajika mitaani. Watu walipopita walinitupia macho tu. Nikawa siambiliki sisemezeki. Si shuleni, si nyumbani. Uvivu ulinijaa nikabaki nikipiga malapa pale nilipoipata nafasi.

Nyumbani nako, wazazi walisema mpaka wakachoka. Majirani nao walibaki tu vinywa wazi kwa kuona vile nilivyokuwa nikijitosa shimoni. Niliwadharau na kuwatweza kupita kiasi. Sikutaka wawe wakifuatilia mienendo yangu. Mimi nilijiona bora si kimaumbile tu lakini hata kifedha. Kiburi kiliota mizizi kipoponi mwangu kwa kuwa nilitoka katika maisha ya fawaishi. Walimu walijaribu kunipa makanyo lakini sikusikia la mwadhini wala la mteka maji msikitini.

Tabia yangu hii ilinifanya niwe na kichwa kikubwa. Nikaanza kuingiwa na matamanio ya kila aina. Shuleni nikawa napatana tu na watu wa aina yangu. Nikajifunza tabia nyinginezo zisizofaa. Nikaanza kulewa na kuvuta visivyotakikana. Tabia hizi zilinifanya nikose makini darasani. Usisahau akili nilikuwa nazo kwelikweli. Hapo awali nilikuwa sipitwi darasani. Ningeshindwa sana ningeambulia nambari tatu darasani. Nilianza kuteremka mlima polepole. Siku za mwisho wa juma na za likizo nilizipenda sana. Badala ya kufanya kazi za likizo, nilizurura kama mbwakoko na wandani wangu wa ubawa mmoja nami. Wazazi waliniasia bila kuchoka lakini maneno yao yalipitia sikio moja na kutokea lile jingine. Wanafunzi waliokuwa makini darasani niliwaona wazuzu wasioijua dunia. Hata niliwacheka kimoyomoyo nilipokuwa nikiwaona wakionyesha tabia zao nyofu kwa walimu na wanafunzi wengine wazuri kama wao.

Siku moja katika hizo pitapita zangu wakati wa likizo, ***nilijiingiza katika ukumbi uliomeza sisisi ya watu na kufura kama andazi lililotiwa hamira***. Nilidhani kuwa huko ningewapata wale wenzangu lakini wapi? Hata hivyo sijui jinsi nilivyoshawishika na kujiunga na watu hao. Nilianza kutulia na kusikiliza yaliyojadiliwa. Mara mmoja wa majirani zangu akapanda jukwaani. Nilitamani kujiondokea lakini badala yake nikaanza kujizungumzia, "Sasa huyu naye ana lipi la kusema mbele ya watu?" Lakini hisia nyingine ikanikanya na kuniambia niache kufuata lisani ya nabii hana heshima kwao.

Amini usiamini, penda ukitaka. Jirani yule ambaye nilikuwa nikimdunisha siku zote kumbe alikuwa na kisima cha nasaha. Ingawa hakuwa ameniona, nilihisi kama aliyekuwa ***akinipiga vijembe***. Alitoa kisa cha mwana mpotevu katika misahafu. Ingawa nilikifahamu kisa hicho, alikisimulia na kukitia chumvi pamoja na bizari duniani, kisiweze kufahamika moja kwa moja ati ndicho hicho. Kisa chenyewe kiliakisi maisha yangu na kiburi nilichokuwa nacho. Nilijiona mwenyewe katika kila sentensi aliyoitamka. Ulimi wa jirani ambaye daima nilimpuuza uliniwekea wazi maisha yangu kama mtazamaji sinema.

Nilijidadisi na kujiuliza maswali chungu nzima. "Mola amenipa kila kitu lakini najididimiza shimoni? Mbona najitia matatani na kuwatia wazazi wangu uchungu na aibu? Mbona sikazani darasani kama zamani? Wakati wa mabadiliko ni huu. Lazima nijikunje mapema kwani hata udongo huwahiwa ukiwa maji.

Kuanzia hapo nikaanza kumthamini yule jirani yangu. Baada ya muda, mabadiliko yangu kitabia yalianza kudhihirika. Shuleni nikaonekana mwana mtiifu. Nilianza kupata alama nilizokuwa nikipata kabla ya maisha yangu ***kutiwa ufa***.

**31.** Kulingana na aya ya kwanza

A. ni msimulizi pekee aliyefaa kuwa na tabia nzuri katika familia yao.

B. jirani aliyedharauliwa na msimulizi alitokea kuwa wa manufaa mengi.

C. msimulizi alifaa kuwa mfano mwema kwa ndugu zake wadogo.

D. msimulizi ndiye aliyekuwa mtoto wa mwisho kuzaliwa.

**32.** Walimu,

A. waliweza kuona mabadiliko ya usimulizi na wakamwadhibu.

B. walionyesha uwajibikaji wa hali ya juu kwa msimulizi.

C. hawakugundua kuwa msimulizi alikuwa na shida.

D. waliwaita shuleni wazazi wa msimulizi ili kuweza kurekebisha tabia zake.

**33.** Shuleni nikawa napatana tu na watu wa aina yangu. Yaani

A. waliokuwa watovu wa nidhamu kama mimi.

B. waliokuwa matajiri kama mimi.

C. waliokuwa wanambee kama mimi.

D. waliokuwa na wanuna kama mimi.

**34.** Ni wazi kuwa

A. matokeo mazuri shuleni huweza kuathiriwa na rubaa.

B. msimulizi hakuwa akielewa chochote darasani.

C. msimulizi alipenda masomo kuliko starehe za mbwa kukalia mkia wake.

D. msimulizi hakuwa na nia yoyote ya kuendelea na masomo.

**35.** Katika shule ya msimulizi

A. wanafunzi wote hawakuwa na nidhamu.

B. wanafunzi wote walikuwa na nidhamu.

C. walimu walikuwa wanashindwa kutekeleza majukumu yao.

D. kulikuwa na wanafunzi ambao walikuwa na misimamo imara ya kuwa waadilifu.

**36.** Kulingana na kifungu

A. mtu unayemwona duni anaweza kuwa msaada mkubwa kwako.

B. msimulizi asingeruhusiwa kufanya mtihani wake iwapo asingebadilisha tabia.

C. watu wote wanaohutubia huokoa maisha ya wasikilizaji.

D. msimulizi hakuwa na tashwishi yoyote kumhusu jirani yake.

**37.** Unadhani kwa nini jirani alitia chumvi kisa cha mwana mpotevu?

A. Hakukielewa vizuri.

B. Hadhira ilikuwa imechoka na kuanza kusinzia.

C. Aliyemsimulilia kisa hicho alikitia chumvi.

D. Alikidhamiria kiwiane na funzo alilokusudia.

**38.** 'Akinipiga vijembe' ina maana ya

A. akinipiga kwa mpini wa jembe.

B. akiniangalia kwa ukali.

C. akizielewa shida zangu.

D. akinisema kwa mafumbo.

**39.** ***<u>Nilijiingiza katika ukumbi uliomeza sisisi ya watu na kufura kama andazi lililotiwa hamira.</u>***

Taja tamathali mbili zinazojitokeza katika kauli hii

A. Janaza, tashbihi.

B. Tashhisi, tashbihi.

C. Chuku, tashbihi.

D. Tashbihi, kinaya.

**40.** ***<u>Kutiwa ufa</u>*** ina maana ya kuwa

A. maisha ya msimulizi yalianza kupata matatizo.

B. maisha ya msimulizi yaliporomoka.

C. maisha ya msimulizi yalianza kubadilika.

D. maisha ya msimulizi yalianza kurekebika.

*Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali 41 mpaka 50.*

Najua si mara moja umemuona mtu akichukua kitabu na kuanza kukisoma vivi hivi tu bila mpangilio wowote. Kile watu wanafaa kuelewa ni kuwa, usomaji ni taaluma tata inayohitaji maandalizi kabambe kabla ya mtu kujitoma katika bahari hiyo. Usomaji chapwa haumfaidi yeyote. Usomaji wowote ule unafaa kumsaidia msomaji kuelewa na kuyakumbuka yale anayoyasoma.

Itambulikane kuwa kabla ya kuanza kusoma, msomaji anafaa kuhakikisha kuwa mahali anaposomea pana mwangaza wa kutosha. Vilevile pahali penyewe panafaa kuwa hapamsumbui msomaji. Usumbufu wa aina yoyote huvuruga mkondo wa kuelewa ayasomayo. Hii ni kwa sababu unapotaka kusoma, mawazo yanatakiwa kulenga unachokisoma. Hivyo basi unahitaji mazingira shwari na yenye utulivu wa moyo na akili.

Baada ya kuteua mahali pa kusomea, lazima msomaji ateue na kuweka wazi lengo la usomaji wake. Ukweli ni kwamba usomaji una malengo mengi na kila lengo lahitaji mwelekeo tofauti na mwingine. ***Mathalani*** lengo la usomaji laweza kuwa ni kusoma mada maalum ili kupata mwanga zaidi baada ya mdahalo mkali kuhusu mada hiyo. Aidha lengo la usomaji laweza kuwa ni kujiburudisha.

Baada ya kuteua lengo, ni vyema ajue ni nini anachotaka kukisoma ili kufikia lengo lake. Inaweza kuwa ni kitabu cha uwanja mahususi kama vile ufundi, matibabu, siasa au makala ya kitaaluma, majorida na kadhalika. Uteuzi wa hicho anachotaka kukisoma kuteuliwa zaidi na lengo la usomaji. Ukurasa wa yaliyomo katika kitabu utamwauni sana msomaji kama huyu kwani ataweza kuipata mada hiyo kwa urahisi. Faharasha iliyomo mwanzoni au mwishoni mwa kitabu nayo itamrahisishia msomaji kurejelea na kupata mada yake kwa urahisi.

Huenda msomaji amebanwa na muda na angetaka kujua kama kitabu kitamsaidia kupata ujumbe autakao. Anaweza kusoma iksiri yaani ufupisho wa yaliyomo, dibaji na utangulizi wa kitabu. Vilevile ni vizuri pia kusoma blabu. Haya ni maelezo yalio nyuma ya jalada la kitabu. Vichwa vya mada kubwa na mada ndogo navyo vinaweza kumwashiria msomaji kama kitabu kina ujumbe autakao.

Ufikapo wakati wa kusoma, yafaa msomaji ajiulize maswali kadhaa kuhusu yale anayoyasoma. Maswali haya yafaa kujibiwa kwa kuandikiwa muhtasari msomaji anapoendelea kusoma. Mtindo huu wa kujiuliza na kuandika humsaidia msomaji kuzingatia lengo la usomaji wake na pia kumpa maandiko anayoweza kuyarejelea baadaye. Ni muhimu msomaji kubuni hati mkato yake ambayo ataitumia na ataielewa hapo baadaye ili kuokoa wakati.

Lengo la msomaji pia hutawala kasi ambayo msomaji atakuwa nayo wakati wa kusoma. Kwa mfano, kusoma kwa minajili ya kujiburudisha kunahitaji kasi. Usomaji wa ufahamu nao huhitaji uangalifu na makini sana. Haya hufaa kutelekezwa kwa makini bila kazi kubwa. Vilevile kasi ya usomaji hutawaliwa na kiwango cha ujuzi alicho nacho msomaji.

**41.** Ni wazi kuwa
A. watu wote wanaojua kusoma husoma bila mpangilio wowote.
B. ni mara moja tu mtu anaweza kuchukua kitabu na kusoma.
C. usomaji ni elimu inayopatikana kwa kusoma na haihitaji kupapia.
D. si lazima usomaji uwe na kigezo chochote.

**42.** Iwapo ulikuwa ukisoma kitabu, halafu ukasikia mayowe
A. kuna uwezekeano kwa kushambulwa na mahasimu.
B. kuna uwezekano mkondo wa kuyapata yale ulikuwa ukisoma utavurugika.
C. kuna uwezekano utasingiziwa kuhusika katika kusababisha vurugu.
D. wafaa kuacha kusoma na kujificha ili kunusuru maandishi yako.

**43.** Usomaji una malengo mengi na kila lengo
A. lahitaji mwelekeo tofauti na mwingine.
B. lahitaji mwelekeo sawa na mwingine.
C. lafanana na malengo yale mengine.
D. si muhimu kama msomaji mwenyewe.

**44.** Faharasa
A. hupatikana mwanzoni pa kitabu pekee.
B. ni muhimu sana kwa msomaji na hupatikana mwishoni mwa kitabu pekee.
C. ni maandishi yanayopatikana kwenye jalada la kitabu.
D. husaidia katika kuokoa wakati unapotafuta mada utakayo.

**45.** Mtu aliyebanwa na wakati anaweza kuokoa wakati kwa kutumia yafuatayo ila
A. kusoma ufupisho wa yaliyomo.
B. kusoma maelezo yaliyo nyuma ya jalada la kitabu.
C. kusoma mada zote ndogo na kubwa.
D. kumtambua mwandishi wa kitabu iwapo ni mashuhuri au la.

**46.** Dhima ya muhtasari katika usomaji
A. ni kudhibiti lengo la usomaji lisipotee.
B. ni kuokoa wakati wa kusoma hususan wakati kuna uchovu.
C. ni kutoa maelezo mafupi na marefu kuhusu mada husika.
D. humwezesha msomaji kuelewa haraka yale anayoyasoma.

**47.** Mambo mawili yanayotawala kasi ya usomaji ni
A. uchovu, nguvu.
B. ujuzi na lengo.
C. afya na lengo.
D. lengo na utamaduni.

**48.** Hati mkato hutumika pale
A. msomaji ana muda wa kutosha wa kukisoma kitabu chake.
B. maandishi ya kitabu si wazi na yanakanganya.
C. msomaji amebanwa na wakati.
D. panafaa kuwa na ushahidi wa yale uliyoyasoma.

**49.** Mathalani ina maana ya
A. kwa mfano.
B. hivyo basi.
C. ingawa.
D. huenda.

**50.** Chagua mada ifaayo kifungu hiki
A. Mbinu za usomaji bora.
B. Faida ya usomaji bora.
C. Manufaa ya usomaji aali.
D. Sifa za usomaji bora.